



# ACCESS

## Kutoa fursa ya upatikanaji wa Elimu ya Msingi kwa watoto walio katika mazingira magumu



actionaid
tanzania

actionaid tanzania

ActionAid Tanzania ni shirika la kimataifa lisilokuwa la kiserikali lililodhamiria kupambana, kwa kushirikiana na jamii, ili kuufanya ulimwengu mahali pazuri pa kuishi, katika kuondoa umaskini, dhuluma na kutokuwa na usawa. Katika kufikia lengo hili, ActionAid Tanzania imekuwa ikifanya kazi na jamii za vijijini nchini Tanzania tangu mwaka 1998 katika kuboresha upatikanaji wa elimu, kupambana na janga la UKIMWI, kutoa nafasi kwa jamii maskini kuboresha maisha yao.

© 2002 ActionAid Tanzania

# ACCESS

## Kutoa fursa ya upatikanaji wa Elimu ya Msingi kwa watoto walio katika mazingira magumu

**ACCESS** ni kifupi cha maneno ya Kiingereza yenye maana ya "Utoaji wa Elimu inayofaa kwenye vituo maalumu kwa kufuata mfumo wa kawaida wa shule na kwa gharama nafuu." Lengo kuu la ACCESS ni kutoa elimu ya msingi kwa watoto, kwa njia inayofaa, inayoweza badilika na kwa gharama nafuu. Watoto wanaosoma katika vituo vya ACCESS hatimaye hujiunga katika mfumo wa shule za kawaida.

ACCESS siyo mfumo mbadala au wa ushindani wa elimu. ACCESS ni mfumo wa ukamilishaji ambao unalisha na kuimarisha mfumo wa kawaida wa shule. Lakini tofauti na shule za kawaida, ACCESS hutumia mtindo unaoweza kubadilika badilika ili kuendana na mahitaji ya watoto wanaoishi katika jamii maskini au mazingira magumu.

Masomo hufundishwa katika vituo vya ACCESS ambavyo vipo ndani ya kijiji. Hii hufanya elimu ya msingi ipatikane kwa urahisi kwa watoto walio na umri wa miaka 7 hadi 14. Programu hii ya kijamii pia huwasaidia wasichana kupata elimu kwa



*Wanafunzi wenye shauku Hawakati tamaa kwa sababu ya kukosa wa samani.*

urahisi kwa sababu familia zinakuwa na uhakika kwamba binti zao wako salama wanapokuwa katika mazingira ya kijiji chao. Vituo huwa vina ushirikiano wa karibu na shule za Msingi za kawaida, na vinatumika kama matawi ya shule hizo. Vituo vya ACCESS havidai watoto wavae sare za shule au kutoa michango ya aina yo yote ile. Hii hupunguza gharama za elimu bila kuathiri ubora wake.

## Kuwafikia Watoto walio Nje ya Shule

"Baada ya miaka miwili tu ya kusoma katika kituo cha ACCESS cha Rugunga, sasa binti yangu Asha anaweza kusoma taarifa zilizoandikwa kwenye kadi ya kliniki ya mdogo wake wa kiume na kumkumbusha mama yake tarehe ya kurudi tena hospitalini kuonana na daktari." Bw. Iddi Mkwafi wa

***Kila mwaka wa masomo ambao mtoto anasoma, huongeza nafasi yake ya kuondokana na umaskini.***



*Maelfu ya familia haziwezi kuwapeleka watoto wao katika shule za kawaida.*





*Wasichana wanaosoma katika vituo vya ACCESS ni nuru inayoibuka ya mfano mzuri katika jamii.*

kitongoji cha Machazo, mkoani Kigoma, anafurahi kwa sababu sasa binti yake anaweza kusoma na kuandika. Muda mfupi uliopita, jambo hili lisingewezekana. Sawa na familia nyingi mkoani humo, Bw. Mkwafi hakuweza kupata ada mbalimbali zilizohitajika katika shule za kawaida - ada, sare, vitabu, na michango kwa ajili ya ujenzi wa shule na ukarabati. Hata pale ambapo familia inaweza kujitolea kwa hali na mali na kulipa ada, bado shule zilikuwa mbali toka kijijini, na hivyo kuwalazimisha watoto kutembea umbali mrefu, wakati mwingine wakipita katika maeneo yenye wanyama wa mwituni. Pia familia maskini zilihitaji watoto wao wasaidie shughuli za kilimo na uzalishaji mali.

ActionAid Tanzania ilifanya utafiti katika mikoa ya Kigoma na Lindi ili kujua kwa nini watoto wengi hawakuwa na fursa ya kupata elimu ya msingi. Umaskini ulionekana ni sababu kubwa ya watoto kunshindwa kwenda shule. Aidha, idadi kubwa ya watoto waliacha shule kabla ya kumaliza elimu yao ya msingi. Jamii zilieleza kwamba uandikishaji duni wa watoto na kuacha shule kulisababishwa na:

- Wazazi kushindwa kutimiza mahitaji ya lazima ya shule kama vile vifaa vya kuandikia, ada na sare.
- Umbali mrefu watoto waliopaswa kutembea hadi shuleni; na
- Ratiba ngumu zisizobadilika ambazo haziwaruhusu watoto kushiriki kazi za nyumbani.

Jamii pia iliona kwamba walimu hawakuwa na ari katika kazi yao na wazazi hawakuwa na kauli katika uendeshaji wa shule. Pia waliona kwamba mtaala haukuwa unafaa kwa maisha ya watoto wao.

Wanavijiji katika kata za Ilagala na Makata waliamua kufanya kitu fulani kwa ajili ya elimu ya watoto wao. Baada ya kuchambua matatizo, walikubali kupokea mfumo wa ACCESS ambao waliamini kwamba ingewapatia watoto wao fursa ya kupata elimu.

## Vituo vya ACCESS

Jamii hujenga vituo vya ACCESS. Vituo hivyo vinajengwa katika vitongoji. Kiwango cha chini kabisa cha kuanzisha darasa la ACCESS ni watoto nane. Viongozi wa kijiji huwaelekeza wananchi namna ya kufanya sensa ya watoto wasioenda shule. Kutokana na taarifa hiyo, wananchi wenyewe huamua kituo kijengwe wapi na pia huchagua kamati ya uongozi wa kituo cha ACCESS.

Katika kila hatua ya kuanzisha kituo, halmashauri ya kijiji, waratibu elimu kata, walimu wakuu wa shule mama za jirani na viongozi wengine wa serikali hupewa taarifa. Aidha, maamuzi ya mwisho hufikiwa na kutekezwa na wanakijiji. Kufanya hivyo husaidia kuhakikisha kwamba vituo vya ACCESS vinamilikiwa, vinaongozwa na vinasaidiwa kwa kamilifu na kijiji.

Jamii hutoa majengo ambayo yanajengwa kwa kutumia vifaa vya gharama nafuu vinavyopatikana kijiji hapo. Madarasa huweza kujengwa kwa udongo na kuezekwa kwa nyasi. Aidha, madarasa





*Vituo vichache tu vinaendeshwa katika majengo ya kudumu na vina samani.*

ya ACCESS yanaweza kufanyika mahali po pote pa kufaa katika eneo hilo, zikiwemo nyumba za watu binafsi, makanisa au misikiti.

Kalenda ya kituo na muda wa vipindi hubadilika badilika na hupangwa na jamii. Pia mtindo huu husaidia kuhakikisha kwamba masomo ya watoto hayaingiliani na majira yale wanapohitajika kulima na kuvuna. Kwa wastani vipindi hufanyika kwa muda wa saa 3-4 kila siku kwa, siku tano kwa wiki. Kila siku muda wa vipindi hubadilika ili kuendana na shughuli za jamii. Kwa mfano, nyakati za masika, vipindi huweza kufanywa mchana tu au kusimamishwa kwa muda mfupi. Idadi ya juu kabisa ya watoto katika darasa ni 40, ambayo hutoa mazingira mazuri ya kufundishia na kujifunzia.



*Watoto hawahitaji kuvaa sare ili waweze kusoma katika kituo cha ACCESS.*

Kwa mfumo wa zamu, jengo moja huweza kutumiwa na watoto wengi zaidi bila kuhitaji vyumba vya ziada. Katika kupunguza zaidi gharama za elimu, watoto wanaosoma katika vituo vya ACCESS hawavai sare.

**Mtaala:** Vituo hufuata mtaala wa taifa, lakini pia hutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia ambazo zinafaa kwa watoto wa kijijini. Wahitimu wa vituo vya ACCESS hukubalika kabisa katika mfumo wa shule za kawaida, mara nyingi wanafanya vizuri zaidi kuliko watoto wa shule za msingi za kawaida.

### Mambo ya Kuzingatia

1. Ushiriki wa jamii
2. Mwanafunzi ndiyo kiini
3. Ratiba inayoweza kubadilika
4. Gharama ndogo kwa familia
5. Kuunganishwa na shule mama
6. Kuhusishwa na shughuli za maendeleo
7. Hutoa fursa wa wasichana na wavulana
8. Mtaala unaofaa
9. Kutumia vifaa vya kiasili
10. Kusaidiwa na jamii
11. Madarasa yawe karibu



## Wawezeshaji wa ACCESS

Wawezeshaji huwafundisha watoto na huendesha vituo vya ACCESS. Ni wataalamu wanaofanyakazi kwa misingi ya muda wa ziada na kujitolea. Ni wanajamii ambao wanaainishwa na huchaguliwa kutoka ndani ya jamii, na jamii yenyewe. Sifa za kuwa mwezeshaji ni za kawaida na hutaegemea uhaba au upatikanaji wa watu wasomi katika eneo husika. Aidha, kiwango cha elimu ya darasa la saba ni sifa ya chini kabisa inayohitajika kwa mwezeshaji kufundisha kwenye kituo cha ACCESS.



*Kwa wawezeshaji wengi programu ya ACCESS ni fursa ya kuendeleza kisomo chao maishani.*

Mafunzo kwa wawezeshaji ni jambo muhimu katika programu ya ACCESS. Hii husaidia kuongeza ubora wa mfumo wa kufundisha-kujifunza na ufanisi au kushindwa kwa programu. Wakufunzi toka katika vyuo vya karibu vya ualimu, walimu wakuu wa shule za msingi mama, waratibu elimu kata na ActionAid Tanzania, huendesha

**Kufundisha Kamiyovu**

***Sofia Stefano ana cheti cha elimu ya sekondari. Alipoolewa na kuhamia Kamiyovu, kwa mshangao wake hapakuwa na shule yo yote au maktaba katika maeneo jirani. Alifikiri kwamba maisha yake ya kusoma yamekwisha hadi kituo cha ACCESS kilipoanzishwa katika kijiji chake. Yeye anasema, "Kituo kimenipatia nafasi ya kutumia maarifa na ujuzi wangu kwa kuwafundisha watoto katika jamii yangu. Ninafurahi na ninaridhika kwa sababu wanajamii wote wanathamini mchango wangu".***



*Wakati wa mafunzo wawezeshaji hutengeneza vifaa vya kujifunzia na kufundishia ambavyo vinaatumika katika kituo cha ACCESS.*

mafunzo. Wawezeshaji hujifunza mbinu za ufundishaji, saikolojia ya watoto, kuandaa vipindi, na jinsi ya kufanya tathmini ya maendeleo ya watoto. Pia wanajifunza jinsi ya kuendesha vituo vya ACCESS na jinsi ya kuihamasisha jamii inayowazunguka kuhusu masuala ya elimu.

Maafisa elimu wa wilaya hupata nafasi ya kuwafundisha wawezeshaji kila baada ya miezi mitatu, kwa muda wa wiki moja. Mafunzo hayo huimarishwa kwa mikutano ya kila wiki na waratibu elimu kata. Mara moja kwa mwaka wawezeshaji wanahudhuraia kozi ya wiki tatu katika chuo cha Ualimu.

Kazi na wajibu za mwezeshaji haziishii katika kufundisha darasani tu. Anatarajiwa pia kukuza ufahamu na kuihamasisha jamii inayomzunguka kuhusu masuala ya elimu, na kujenga uhusiano mzuri na wazazi kwa kuwatembelea majumbani. Pia mwezeshaji ni katibu wa kamati ya ACCESS inayoongoza Kituo.

## Rasilimali ya Jamii

Mafanikio ya programu ya ACCESS siyo tu elimu kwa watoto. Lengo la mwisho ni kujenga msingi kwa umiliki wa jamii wa kuwa na taasisi ya elimu kwa gharama nafuu, zinazofaa na zinazoweza kubadilika. Mfumo huu hukuza uwezo wa jamii wa kuongoza na kuendeleza programu za ACCESS hapo baadaye.

Vituo vya ACCESS huongozwa na Kamati maalumu. Kamati inakuwa na wajumbe 4 au 5 pamoja na mwezeshaji wa kituo. Wazazi ndio wanaowachagua wajumbe wa Kamati, ambao



lazima wawe watu wanaoheshimika katika jamii na ambao wapo tayari kusimamia shughuli za kituo. Katika kuongeza mbinu za utawala wajumbe wa Kamati hupata mafunzo toka kwa afisa elimu wilaya.

Jamii, kwa kusaidiana na Kamati ya kituo, inawajibika katika:

- kuchagua, kutoa mafunzo na kuwafuatilia wawezeshaji;
- kujenga vituo vya ACCESS;
- kuhakikisha mahudhurio ya kudumu ya watoto wao;
- kukusanya vifaa kufundishia na kujifunzia; na
- kuwalipa wawezeshaji.



*Kujenga Kituo ni kazi ya pamoja.*

Wazazi wanahimizwa kutoa vifaa vya kufundishia kama vile kalamu na daftari lakini hata wale watoto wasiokuwa na vitu hivi, wanaruhusiwa kuhudhuria vipindi vyote.

Kamati hujiwekea taratibu zake na huhakikisha wazazi wanatekeleza majukumu yao. Kamati husimamia kazi za wawezeshaji, kwa kuhakikisha kwamba wanahudhuria vipindi vyao vyote. Katika mikutano ya kamati ya kila wiki, wajumbe hujadili mahudhurio na maendeleo ya watoto na masuala yanayohusiana na majengo. Kamati hufanya kazi pamoja na mwalimu mkuu wa shule ya msingi mama na Mratibu Elimu Kata, katika:

- kupanga ratiba ya kila siku na kalenda ya mwaka ya vipindi;
- kukusanya vifaa vya kufundishia na kujifunzia toka kwa afisa elimu wilaya, shule ya msingi mama na mashirika husika yasiyokuwa ya kiserikali; na
- kutathmini maendeleo ya watoto.

Kila mwezi Kamati ya ACCESS huwaalika wazazi na Mratibu Elimu Kata kupokea ripoti za maendeleo ya watoto na hali ya majengo. Pia wazazi hujifunza jinsi ya kuwasaidia watoto wao ili wawe na maendeleo mazuri.

Kamati ni kiungo kati ya jamii na shule ya msingi mama na mwalimu mkuu. Waratibu Elimu Kata, halmashauri ya wilaya, ActionAid Tanzania na mashirika husika mengine yasiyokuwa ya kiserikali. Kamati hufuatilia masuala yale yaliyopendekezwa na maafisa elimu. Mara mbili kwa mwaka Kamati ya wazazi hukutana na maafisa elimu kutathmini maendeleo ya jumla ya programu ya ACCESS na kufanya mipango kwa miezi sita inayofuata.

***Mzee Athumani Kiboko, Mwenyekiti mstaafu wa kijiji, anaumia sana kuona watoto wengi hawaendi shule.***

***"Kuna shule moja tu hapa kijijini yenye wanafunzi 600. Lakini kuna watoto zaidi ya 500 wenye umri wa kwenda shule ambao wanashindwa kwenda shule kwa sababu wanaishi vijiji vya mbali, kilomita saba kutoka shuleni hapo.***

***Tulipata kufahamu kuhusu programu ya ACCESS kutoka kijiji cha jirani. Hatukupata shida kuhamasisha wana kijiji wenzetu kujenga madarasa na kuchangia shilingi 200 kwa wawezeshaji, kwani ndicho kitakachowezesha watoto wao kupata elimu.***

***Kila mtu anapenda mtoto wake aende shule. Hivi sasa kuna watoto 400 katika vituo hivi vya ACCESS. Tumefanikiwa kuongeza zaidi ya watoto 1000 kwenye vituo hivyo".***



## Kutoa Matumaini kwa Mustakabali Mwema

Tangu mwaka 1999, watoto 4,356 - waqsichana 2150 na wavulana 2206 - ambao walikuwa na tumaini dogo sana la kupata elimu, wamesoma katika vituo 32 vya ACCESS. Upatikanaji wa elimu ya msingi katika wilaya za Kigoma na Liwale vijijini, umepanda kutoka asilimia 16 na 27 mnamo mwaka 1998 hadi asilimia 76 na 80 mnamo mwaka 2002. Idadi ya watoto wanaoacha shule pia imepungua kwa kiasi kikubwa. Wawezeshaji 116 wamekuwa wakiwafundisha watoto na kuendesha vituo vya ACCESS.


**Programu inayoweza kubadilika:** Watoto wanaosoma katika vituo vya ACCESS wana umri wa miaka 7 na 14. Aidha, katika vituo vingine watoto wenye umri wa 15 wamejiunga na programu hii. Kwa hiyo, tofauti na shule za msingi za kawaida ambako umri wa miaka 7 imewekwa kama sharti la kuandikishwa darasa la kwanza, programu ya ACCESS hutoa urahisi kwenye sharti la umri. Sharti moja tu muhimu la kuandikishwa ni hiari ya mtoto ya kusoma.

Viwango vya madhuhurio vya watoto katika vituo ni vya juu sana. Muda unaobadilika ili kuhahakikisha kwamba watoto hawana kazi za ushindani za kufanya nyumbani, na wakati huo



*Muda wa masomo huzingatia mazingira na mahitaji ya nguvu kazi ya watoto kwenye jamii. Kwa sababu hii wazazi huhamasika kuandikisha watoto wao katika vituo vya ACCESS.*

huo pia wanahitajika darasani. Vipindi huwa havifanyiki wakati wa majira yale ambapo watoto na familia zao wanakabiliwa na shughuli nyeti majumbani. Viwango vya kuacha shule ni vya chini zaidi kuliko vile vya shule za msingi za kawaida. Mama Sofia Stefano, mwezeshaji wa Kituo cha ACCESS cha Kamiyovu huko Ilagala, anathibitisha kwamba ACCESS imeleta tofauti katika maisha ya wasichana katika kijiji hicho. "Hivi sasa idadi ya wasichana wanaoolewa au wanaopata mimba katika umri mdogo ni ndogo sana. Wasichana wengi hawapendi




*ACCESS imempatia Mfaume Ngemba fursa ya kujiendeleza.*

**Mfaume Ngemba: Kuweka malengo katika midani ya kitaifa**


**Atakapokua, Mfaume atapenda kuwa mwanasiasa - labda hata rais wa Tanzania. Kwanini? Anasema, "Kama rais nitaweza kutembea nchi nzima na kukutana na watu wengi. Pia ninaweza kufanya maamuzi muhimu ambayo yatakuwa na faida kwa watu wote, hasa watoto", ari ya Mfaume haionyeshi vihunzi anavyopaswa kupanda ili kupata elimu.**

**Wazazi wajitahidi kuweka akiba kwa ajili ya kumsomesha mtoto wao, hivyo walimwandikisha katika shule ya msingi ya Mlembwe. Aidha, baada ya muda si mrefu walilazimika kumwachisha shule. Kwa sababu familia ya Mfaume ilikuwa ikiishi katika kijiji cha Mlembwe, kata ya Makata, ilimpasa atembee kwa miguu kilomita 11 kila siku ili aweze kufika shule ya msingi ya iliyokuwa jirani. Wazazi wake iliwapasa wafikie uamuzi mgumu wa kumwachisha shule Mfaume kwa usalama wake. Lakini baada ya kufunguliwa kituo cha ACCESS katika kijiiji cha Nambinda, Mfaume aliendelea na elimu yake. Kutokana na kutiwa moyo na wazazi wake na jitihada zake binafsi, amejipatia sifa kubwa sana. Matokeo yake ya darasa la pili yalikuwa ya juu sana katika kata yote ya Makata katika mwaka 2002. Mfaume na wazazi wake wamepania kutovurauga mafanikio haya ya awali kutoka katika shabaha yake - kujipatia elimu ya chuo kikuu.**



kukatisha masomo yao na wamekuwa mfano mzuri wa kuigwa kijijini."

Watoto wanaohitimu kisomo chao cha msingi katika vituo hivi, hufanya mitihani ya taifa ya darasa la nne. Watoto wengi wanafaulu zaidi ya watoto wenzao wa shule za msingi nyingine.



*Wawezeshaji wenye nia wamewahamasisha watoto kusoma kwa bidii.*

**Wawezeshaji wenye nia:** Miongoni mwa sababu zinazochangia kuwa na matokeo mazuri ya wahitimu wa ACCESS ni uwiano wa chini wa mwezeshaji na wanafunzi, ufuatiliaji wa karibu wa kituo unaofanywa na jamii na uwajibikaji wa wawezeshaji kwa Kamati ya ACCESS na jamii.


Msaada wanaopata wawezeshaji ni kitu kidogo sana ukilinganisha na kazi wanayofanya. Jamii zinawashukuru wawezeshaji kwa ari yao thabiti na motisha yao. Bw. Ezekiel Kazyogo wa kituo cha ACCESS cha Kabeba katika wilaya ya Kigoma vijijini, anafurahi kutoa huduma yake kwa ajili ya watoto. "Kufundisha katika vituo vya ACCESS inafurahisha sana. Kuwapatia watoto nafasi ya kujifunza na kuona jinsi walivyo na ari ya kupata kitu fulani kipya kila siku ni thawabu kubwa sana.

***"Sasa ninaweza kusoma na kuandika. Ninapenda shule kwa sababu ipo karibu na nyumbani kwangu. ACCESS ni mkombozi wangu na kwa dada zangu wawili. Kaka zangu na dada zangu wakubwa walisoma mpaka darasa la tatu tu".***
***- Zubeda Ahmed, mtoto wa sita wa Ahmed Baruani.***

Ni jambo zuri zaidi kuliko kiasi cho chote cha fedha wanazoweza kunipatia wanakijiji."

Watoto wanahamasishwa kusoma kwa bidii wanapoona ari kubwa ya mwezeshaji wao. Watoto katika vituo vya ACCESS wamekuwa wakilipa fadhila kwa wawezeshaji kutokana na jitihada zao. Zaidi ya watoto 500 wanaohamishiwa katika shule za msingi wanafaulu vizuri sana kiasi kwamba wanapandishwa kwenye madarasa ya juu kuliko wenzao wenye umri sawa nao katika shule za msingi.

**Ubia wenye manufaa:** Fahari ya kituo cha ACCESS ni mchanganyiko wa ubia unaoweza kuundwa. Vituo vya ACCESS hujenga kwa urahisi uhusiano wenye nguvu na shule za msingi za jirani katika kushirikishana uzoefu na kujifunza toka kila upande. Walimu wakuu wa shule za msingi mama wanavisaidia vituo vya ACCESS kwa vifaa na mara nyingi hutoa muda wao kuwasaidia wawezeshaji wa ACCESS wanapohitaji msaada wa ziada.



*Wazazi wanauhakika na usalama wa watoto wao wa kike wasomao karibu na nyumbani.*

Ubia kati ya wawezeshaji na wazazi ni ufunguo kwa kisomo chenye faida. Ushirikiano miongoni mwa wazazi, wawezeshaji na wanafunzi huhakikisha kwamba watoto wanakuwa na maendeleo mazuri. Watoto wanapata ari ya kujifunza wanapoona wazazi wao wanapenda na wanajihusisha katika elimu yao na katika uendeshaji mwororo wa vituo vya ACCESS. Mafanikio ya mfumo wa elimu katika vituo vya ACCESS ni changamoto kwa shule za kawaida. Jamii nyingi zimeomba msaada toka ActionAid Tanzania wa kuanzisha vituo katika vijiji vyao.





*Maofisa wa serikali huvitembelea vituo kukagua ubora wa mafunzo.*

Maofisa elimu wa wilaya wameona mafanikio ya vituo hivyo. Maofisa elimu wametenga fungu la msaada wa fedha katika bajeti zao kwa ajili ya vituo vya ACCESS na mara kwa mara hutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Mara nyingi za msingi za wanapofanya ziara za ukaguzi katika shule kawaida, pia huvitembelea vituo vya ACCESS. Ubia na Wazara ya Elimu na

***Kata nzima ina watoto 3,400 wanaosoma. Kati ya hao 1,250 wanasoma katika vituo 13 vya ACCESS. Watoto walio katika vituo vya ACCESS hawakuweza kwenda katika shule za msingi za kawaida kwa sababu shule hizo zipo umbali wa kilomita kati ya 5 hadi 13.***

***Huwa ninafanya ziara ya kuvitembelea vituo vya ACCESS mara nne kwa mwaka, na nimeona kwamba watoto wana maendeleo mazuri sana. Vituo vitatu vimepandishwa kuwa shule za msingi.***

***Mtindo wa Elimu wa ACCESS umefanikiwa kwa sababu jamii inahusishwa katika kupanga kalenda ya shule na masuala yote yanayohusiana na elimu ya watoto wao. Kwa sasa elimu ya msingi inapatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu kwa familia ambazo zinategemea shughuli za uvuvi.***

***- Mratibu wa Elimu Kata ya Ilagala***

Utamaduni umesaidia katika kupandisha hadhi ya baadhi ya vituo vya ACCESS kuwa shule za msingi katika kata za Makata na Ilagala. Wizara kwa kushirikiana na wahandisi wa wilaya na jamii wanashughulikia taratibu za usajiri na ujenzi wa majengo ya kudumu. Wizara ya Elimu na Utamaduni, pia imechukua mtindo wa ACCESS kwa ajili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM).

Mafanikio ya ACCESS yanaonyesha kwamba jamii zinaweza kutafuta majawabu endelevu kwa matatizo yao. Kwa kupewa maelekezo mazuri, nafasi na kutambuliwa, jamii maskini zina uwezo mzuri tu wa kushughulikia mahitaji yao ya maendeleo. "Huwa sikosi mkutano hata mmoja unaotishwa na Kamati ya ACCESS," anasema Sadiki Issa toka kijiji cha Nambinda huko Lindi. "Katika mikutano hiyo ninapata nafasi ya kutoa maoni yangu na kusikilizwa. Lakini katika shule nyingine ni 'watalaamu' tu ndio wanaozungumza, na kwa muda mrefu. Iwapo hukubaliani na mawazo yao, unaitwa 'mshamba'".



## ACCESS Can Benefit Your Community

Kwa maelezo zaidi kuhusu ACCESS, tafadhali andika kwa:

**Mkurugenzi Mkuu**
ActionAid Tanzania
Mtaa wa Urambo Na.344, Upanga
S.L.P. 21496 Dar Es Salaam, Tanzania

Simu: +255 (0) 22 2150711
Faksi: +255 (0) 22 2151003
Barua pepe: admin@actionaidtz.org